

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI



MAMLAKA YA UDHIBITI WA  
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI  
(EWURA)



**KUMB: PPR/2021 - 01/1**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI  
KUANZIA JUMATANO, TAREHE 6 JANUARI 2021**

Mamlaka ya Udhibili wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 6 Januari 2021**. Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za rejareja na jumla za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyopokelewa kuitia **Bandari ya Dar es Salaam** zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 2 Desemba 2020. Kwa Januari 2021, bei ya rejareja ya Petroli imepungua kwa shilingi 31/Lita (sawa na asilimia 1.67) wakati bei za rejareja za Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 9/lita (sawa na asilimia 0.52) na Shilingi 29/lita (sawa na asilimia 1.81). Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei ya jumla ya Petroli imepungua kwa shilingi 31.10/Lita (sawa na asilimia 1.79) wakati bei za jumla za Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 8.74/lita (sawa na asilimia 0.56) na Shilingi 29.31/lita (sawa na asilimia 1.96), mtawalia.
- (b) Kwa Januari 2021, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kaskazini** (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimebadilika ikilinganishwa na bei zilizotolewa tarehe 2 Desemba 2020. Kwa mwezi Januari 2021, bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa shilingi 31/lita (sawa na asilimia 1.71) na shilingi 61/lita (sawa na asilimia 3.6), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa shilingi 30.59/lita (sawa na asilimia 1.83) na shilingi 60.73/lita (sawa na asilimia 3.88) mtawalia. Hata hivyo, bei za Mafuta ya Taa hazina mabadiliko na zitaendelea kuwa zile zilizotangazwa katika toleo la tarehe 2 Desemba 2020. Hii ni kwa sababu, kwa Desemba 2020 hakuna shehena ya Mafuta ya Taa iliyopokelewa kuitia bandari ya Tanga.
- (c) Kwa Januari 2021, bei za rejareja na jumla kwa bidhaa za mafuta ya

Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kusini (Mtwara, Lindi, and Ruvuma)** zimebadilika ikilinganishwa na bei zilizotolewa tarehe 2 Desemba 2020. Kwa Januari 2021, bei ya rejareja ya Petroli imepungua kwa shilingi 2/lita (sawa na asilimia 0.13) wakati bei ya rejareja ya Dizeli imeongezeka kwa Shilingi 20/lita (sawa na asilimia 1.15). Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei ya jumla ya Petroli imepungua kwa shilingi 2.35/lita (sawa na asilimia 0.14) wakati bei ya jumla ya Dizeli imeongezeka kwa Shilingi 19.91/lita (sawa na asilimia 1.24).

- (d) Mabadiliko haya ya bei yanachangiwa na kubadilika kwa bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji (*BPS Premium*).
- (e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba **\*152\*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (f) Kwa mujibu wa **Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166**, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (g) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu **bei hizo zisivuke bei kikomo (price cap)** kama **ilivyokokotolewa na kanuni (formula)** iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 656 la tarehe 21 Agosti 2020.
- (h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo

kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

#### **JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA**

<b>Mji</b>	<b>Bei Kikomo</b>		
	<b>Petroli (Shs/Lita)</b>	<b>Dizeli (Shs/Lita)</b>	<b>Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)</b>
<b>Dar es Salaam</b>	<b>1,834</b>	<b>1,695</b>	<b>1,650</b>
<b>Arusha</b>	<b>1,885</b>	<b>1,811</b>	<b>2,051</b>
Arumeru (Usa River)	1,885	1,811	2,051
Karatu	1,903	1,829	2,069
Longido	1,896	1,822	2,062
Monduli	1,890	1,816	2,056
Monduli-Makuyuni	1,895	1,821	2,061
Ngorongoro (Loliondo)	1,969	1,895	2,136
<b>Pwani (Kibaha)</b>	<b>1,838</b>	<b>1,700</b>	<b>1,655</b>
Bagamoyo	1,845	1,706	1,661
Bagamoyo (Miono)	1,875	1,737	1,692
Chalinze Junction	1,848	1,710	1,664
Chalinze (Msata)	1,852	1,714	1,669
Kibiti	1,854	1,716	1,671
Kisarawe	1,841	1,703	1,657
Mkuranga	1,843	1,705	1,660
Rufiji	1,861	1,723	1,678
<b>Dodoma</b>	<b>1,892</b>	<b>1,754</b>	<b>1,709</b>
Bahi	1,900	1,761	1,716
Chamwino	1,888	1,749	1,704
Chemba	1,919	1,781	1,736
Kondoa	1,925	1,787	1,742
Kongwa	1,890	1,751	1,706
Mpwapwa	1,894	1,755	1,710
Mtera (Makatopora)	1,911	1,773	1,728
Mvumi	1,899	1,761	1,716
<b>Geita</b>	<b>1,999</b>	<b>1,861</b>	<b>1,816</b>
Bukombe	1,988	1,850	1,805
Chato	2,020	1,882	1,837
Mbogwe	2,037	1,899	1,854
Nyang'hwale	2,014	1,876	1,831
<b>Iringa</b>	<b>1,898</b>	<b>1,760</b>	<b>1,714</b>
Ismani	1,903	1,765	1,720
Kilolo	1,902	1,764	1,719
Mufindi (Mafinga)	1,908	1,770	1,724
Mufindi (Igowole)	1,916	1,778	1,733

<b>Kagera (Bukoba)</b>	<b>2,049</b>	<b>1,911</b>	<b>1,866</b>
Biharamulo	2,023	1,885	1,840
Karagwe (Kayanga)	2,066	1,927	1,882
Kyerwa (Ruberwa)	2,071	1,933	1,888
Muleba	2,049	1,911	1,866
Ngara	2,037	1,899	1,854
Misenyi	2,058	1,919	1,874
<b>Katavi (Mpanda)</b>	<b>2,042</b>	<b>1,903</b>	<b>1,858</b>
Mlele (Inyonga)	2,061	1,923	1,878
Mpimbwe (Majimoto)	2,035	1,896	1,851
Tanganyika (Ikola)	2,060	1,921	1,876
<b>Kigoma</b>	<b>2,065</b>	<b>1,927</b>	<b>1,882</b>
Uvinza (Lugufu)	2,077	1,939	1,894
Buhigwe	2,054	1,916	1,871
Kakonko	2,022	1,884	1,839
Kasulu	2,051	1,913	1,868
Kibondo	2,029	1,891	1,846
<b>Kilimanjaro (Moshi)</b>	<b>1,874</b>	<b>1,800</b>	<b>2,041</b>
Hai (Bomang'ombe)	1,878	1,804	2,044
Mwanga	1,868	1,793	2,034
Rombo (Mkuu)	1,891	1,817	2,057
Same	1,861	1,787	2,027
Siha (Sanya Juu)	1,881	1,807	2,047
<b>Lindi</b>	<b>1,846</b>	<b>1,766</b>	<b>1,709</b>
Lindi-Mtama	1,850	1,771	1,727
Kilwa Masoko	1,869	1,790	1,684
Liwale	1,881	1,802	1,730
Nachingwea	1,866	1,786	1,738
Ruangwa	1,872	1,793	1,740
<b>Manyara (Babati)</b>	<b>1,919</b>	<b>1,845</b>	<b>2,085</b>
Hanang (Katesh)	1,929	1,855	2,095
Kiteto (Kibaya)	1,934	1,860	2,100
Mbulu	1,932	1,857	2,098
Simanjiro (Orkasumet)	1,951	1,877	2,117
<b>Mara (Musoma)</b>	<b>2,012</b>	<b>1,874</b>	<b>1,829</b>
Musoma Vijijini (Busekela)	2,053	1,915	1,870
Rorya (Ingirijuu)	2,021	1,883	1,838
Rorya (Shirati)	2,056	1,918	1,873
Bunda	2,003	1,865	1,820
Bunda (Kisorya)	2,013	1,875	1,830
Butiama	2,009	1,871	1,826
Serengeti (Mugumu)	2,058	1,920	1,875
Tarime	2,023	1,885	1,840
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,028	1,890	1,844
<b>Mbeya</b>	<b>1,941</b>	<b>1,803</b>	<b>1,757</b>
Chunya	1,950	1,812	1,767
Chunya (Makongolosi)	1,965	1,826	1,781

Kyela	1,957	1,818	1,773
Mbarali (Rujewa)	1,925	1,787	1,741
Rungwe (Tukuyu)	1,950	1,812	1,766
<b>Morogoro</b>	<b>1,859</b>	<b>1,720</b>	<b>1,675</b>
Mikumi	1,874	1,736	1,691
Kilombero (Ifakara)	1,896	1,758	1,713
Kilombero (Mlimba)	1,919	1,781	1,736
Kilombero (Mngeta)	1,908	1,770	1,725
Ulanga (Mahenge)	1,907	1,769	1,724
Malinyi	1,917	1,779	1,734
Kilosa	1,877	1,739	1,694
Gairo	1,877	1,739	1,694
Mvomero (Wami Sokoine)	1,869	1,731	1,686
Mvomero (Sanga Sanga)	1,859	1,720	1,675
Turiani	1,884	1,746	1,700
<b>Mtwara</b>	<b>1,832</b>	<b>1,753</b>	<b>1,723</b>
Nanyumbu (Mangaka)	1,868	1,789	1,772
Masasi	1,848	1,769	1,748
Newala	1,853	1,774	1,755
Tandahimba	1,846	1,767	1,748
Nanyamba	1,846	1,767	1,748
<b>Mwanza</b>	<b>1,984</b>	<b>1,846</b>	<b>1,800</b>
Kwimba	2,002	1,863	1,818
Magu	1,992	1,854	1,809
Misungwi	1,978	1,840	1,795
Sengerema	2,016	1,878	1,833
Ukerewe	2,043	1,905	1,860
<b>Njombe</b>	<b>1,926</b>	<b>1,788</b>	<b>1,743</b>
Njombe (Kidegembye)	1,947	1,808	1,763
Ludewa	1,964	1,826	1,781
Makambako	1,918	1,780	1,735
Makete	1,957	1,819	1,774
Wanging'ombe (Igwachanya)	1,924	1,786	1,740
<b>Rukwa (Sumbawanga)</b>	<b>2,007</b>	<b>1,868</b>	<b>1,823</b>
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	2,007	1,868	1,823
Kalambo (Matai)	2,014	1,876	1,830
Nkasi (Namanyelete)	2,020	1,882	1,837
<b>Ruvuma (Songea)</b>	<b>1,918</b>	<b>1,838</b>	<b>1,774</b>
Mbinga	1,930	1,851	1,807
Namtumbo	1,909	1,829	1,803
Nyasa (Mbamba Bay)	1,956	1,876	1,818
Tunduru	1,883	1,804	1,833
<b>Shinyanga</b>	<b>1,963</b>	<b>1,825</b>	<b>1,780</b>
Kahama	1,976	1,838	1,793
Kishapu	1,991	1,853	1,808
Ushetu (Nyamilangano)	1,994	1,856	1,810
Salawe	1,977	1,839	1,794

<b>Simiyu (Bariadi)</b>	<b>2,004</b>	<b>1,866</b>	<b>1,821</b>
Busega (Nyashimo)	1,997	1,859	1,814
Itilima (Lagangabilili)	2,007	1,869	1,824
Maswa	1,995	1,857	1,812
Meatu (Mwanhuzi)	2,003	1,864	1,819
<b>Singida</b>	<b>1,924</b>	<b>1,786</b>	<b>1,741</b>
Iramba	1,936	1,798	1,753
Manyoni	1,909	1,771	1,726
Itigi (Mitundu)	1,924	1,786	1,741
Ikungi	1,920	1,782	1,736
Mkalama (Nduguti)	1,949	1,811	1,766
<b>Songwe (Vwawa)</b>	<b>1,950</b>	<b>1,812</b>	<b>1,767</b>
Songwe (Mkwajuni)	1,957	1,819	1,774
Ileje	1,954	1,816	1,771
Momba (Chitete)	1,959	1,821	1,776
Tunduma	1,954	1,816	1,771
<b>Tabora</b>	<b>1,988</b>	<b>1,850</b>	<b>1,805</b>
Igunga	1,942	1,804	1,758
Kaliua	2,007	1,869	1,824
Ulyankulu	2,001	1,863	1,818
Nzega	1,952	1,814	1,769
Sikonge	2,000	1,861	1,816
Urambo	2,001	1,863	1,818
Uyui	1,989	1,851	1,805
<b>Tanga</b>	<b>1,828</b>	<b>1,754</b>	<b>1,994</b>
Handeni	1,849	1,775	2,015
Kilindi	1,864	1,790	2,030
Korogwe	1,840	1,766	2,006
Lushoto	1,850	1,776	2,016
Mkinga (Maramba)	1,835	1,761	2,001
Muheza	1,833	1,759	1,999
Pangani	1,835	1,761	2,001

### JEDWALI B: BEI ZA JUMLA

	<b>Petroli (Shs/Lita)</b>	<b>Dizeli (Shs/Lita)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Shs/Lita)</b>
DAR ES SALAAM	1,705.80	1,567.62	1,523.23
TANGA	1,700.41	1,626.06	1,866.20
MTWARA	1,704.35	1,624.79	-

**Kapwete Leah John**  
**Kny: MKURUGENZI MKUU**  
**EWURA**